JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

TAKUKURU Mkoa,
S. L. P 845,
MOROGORO,

Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAARIFA KWA UMMA

Morogoro
Februari , 2024

ADAKWA KWA KUMHONGA AFISA WA TAKUKURU

Ndugu WanaHabari,

TAKUKURU Mkoa wa Morogoro ilimkamata na kumfikisha Mahakamani Bw. Suleiman Mwishehe alipojaribu kumhonga afisa wa TAKUKURU aliyekuwa anachunguza tuhuma dhidi za ubadhilifu wa shilingi milioni 90 zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu na ujenzi wa chumba cha darasa katika Kijiji cha Mlilingwa – Tununguo Wilaya ya Morogoro.

Mshtakiwa huyo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi na Mlezi wa Kikundi cha Bosi Kuku Group, alikamatwa baada ya kumpa Afisa wa TAKUKURU kiasi cha Shilingi milioni tatu kati ya milioni tano alizoshawishi awali kuwa yeye na watuhumiwa wenzake watampa ili wasifikishwe Mahakamani.

Mshtakiwa alikiri kosa na kutiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya shilingi laki tano na fedha alizotoa kama hongo kutaifishwa na kuwa mali ya Serikali. Mshatkiwa alilipa faini ya shilingi 500,000.00 na kiasi cha shilingi milioni tatu zilitaifishwa.

Ninatoa ONYO kwa Mwananchi yoyote asijaribu kushawishi au kutoa hongo kwa Mtumishi wa TAKUKURU mahali popote Mkoani Morogoro kwa lengo la kuharibu uchunguzi au ushahidi wa tuhuma zozote zinazochunguzwa na

TAKUKURU. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kama ilivyokuwa kwa Bw.Mwishehe.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU Morogoro katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2023 tumetekeleza majukumu yafuatayo;

1. UZUIAJI RUSHWA

1.1 UFUATILIAJI UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi cha Mwezi **Oktoba 2023** hadi **Disemba 2023,** tumefuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayohusu Elimu, Maji na Mifugo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni Saba (7.29)** ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha kati ya miradi iliyofuatiliwa, miradi 14 yenye thamani ya shilingi Bilioni 6.6 ilikuwa na mapungufu ambapo TAKUKURU imechukua hatua mbalimbali. **(Kiambatisho 1)**

Kwa upande wa udhibiti wa matumizi ya fedha za Umma, tumeweza kuokoa zaidi ya fedha **Shs 124,550,500.** Fedha hizo zilitumika kununua misumari, kofia zake na mabati yasiyokuwa na ubora toka kwa Kampuni ya **KINGLION INVESTMENT** na **BATIBOMBA LTD** waliopewa zabuni ya kusambaza mabati katika shule mpya za Sekondari ya Ruhembe, Muhenda na Madoto zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya Kilosa.

Baada ya TAKUKURU kufuatilia, Kampuni ya BATIBOMBA ilirejesha jumla ya shilingi **55,336,000.00** na kuchukua bati 1088, kofia 86 na misumari Kg. 201 vifaa ambavyo kampuni hiyo ilikuwa imepeleka katika Shule ya Sekondari Madoto. Kampuni ya KINGLION INVESTMENT ilirejesha shilingi **69,214,000.00** na kurejeshewa mabati 1094, kofia 106 na misumari Kgs. 226 ambazo Kampuni hiyo ilikuwa imepeleka katika shule ya Sekondari Ruhembe, Zahanati ya UNONE na shule ya Sekondari Muhenda.

Ninachukua fursa hii kuwakumbusha wazabuni wote wanaoingia mikataba na Serikali katika kuuza vifaa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo Mkoani Morogoro, kuuza vifaa vinavyozingatia ubora.

Aidha watumishi wa umma ambao wamepewa dhamana ya kufanya manunuzi ya vifaa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuhakikisha wananunua vifaa vyenye ubora kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyowekwa na

Serikali. TAKUKURU itachukua hatua za kisheria kwa wote watakaopatikana na makosa katika zoezi zima la utekelezaji wa miradi ya maendeleo.-

1.2 UCHAMBUZI WA MIFUMO

Katika kipindi cha **Oktoba 2023** hadi **Desemba 2023** TAKUKURU Mkoa wa Morogoro tumefanya chambuzi za mifumo **4.** Katika chambuzi hizo, chambuzi tatu (3) zilihusu mianya ya rushwa katika huduma zinazotolewa katika sekta ya ardhi na chambuzi moja ilihusu mianya ya rushwa katika uendeshaji wa minada ya mifugo katika Halmashauri. (Kiambatanisho 2).

2. ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi tajwa, kupitia Dawati la Elimu kwa Umma, tumeweza kufanya jumla ya Mikutano ya Hadhara **46,** semina **41** kwa wananchi, watumishi wa umma na wa sekta binafsi, tumeimarisha klabu za wapinga rushwa wa shule za msingi, sekondari na vyuo **69,** tumeandaa na kurusha vipindi vya Redio na TV **04,** uandishi wa makala **08, Onesho 01.**

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Kwa upande wa uchunguzi tumepokea jumla ya malalamiko **109,** kati ya hayo, malalamiko **70** yalihusu vitendo vya rushwa na uchunguzi wake uko katika hatua mbalimbali na malalamiko **39** hayakuhusu rushwa. Malalamiko ambayo hayakuhusu rushwa walalamikaji walishauriwa na wengine kupelekwa kwenye mamlaka husika.

Aidha, sekta zilizolalamikiwa ni kama ifuatavyo:Tamisemi/Watendaji wa Vijiji/Mitaa na Kata **26,** Elimu **23**, Ardhi **13**, Mahakama **08**, Ujenzi **07**, Vyama vya Ushirika/Saccos **06**, Afya **05,** Taasisi za fedha **05**, Kilimo **05,** Polisi **(05),** Maji **03**, Maendeleo ya Jamii **02** na Misitu **01**.

Kesi Mpya	Kesi zilizoamuliwa	Kesi zilizoshinda	Kesi kushindwa/ Ondolewa	Kesi zinazoendelea Mahakamani
08	05	02	03	11

Utekelezaji wa PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

Katika kutekeleza Programu ya TAKUKURU Rafiki, ofisi ya TAKUKURU (M) Morogoro imetoa mrejesho kwa wananchi kuhusiana na kero walizoziibua katika mikutano iliyopita. (**Kiambatisho 3**).

Aidha, tumeendelea kushirikiana na wadau kutoka kwenye sekta mbalimbali na tumeweza kuzifikia kata 13 na kuibua kero 81 na kero 42 zilitatuliwa. Tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia mianya ya rushwa kwani utatuzi wa kero hizo hupelekea upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi na kukuza ushirikiano kati ya TAKUKURU, wananchi na wadau wanaohusika katika kutoa huduma **(Kiambatisho 4)**

MIKAKATI YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI MACHI 2024.

Katika kipindi tajwa tumejiwekea mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kwanza, ifahamike kuwa mwaka **2024** ni mwaka wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo viashiria vingi vya rushwa huanza kujitokeza kabla ya muda ambao utatangazwa na Tume ya Uchaguzi. Hivyo tumeanza kufuatilia vitendo hivyo ili tuweze kuchukua hatua mbalimbali za kisheria kwa watakaobainika.

Pili, tutatoa elimu ya uzuiaji wa vitendo vya rushwa kwa wananchi hasa kipindi hiki ambacho wananchi wanajiandaa kushiriki katika chaguzi za upatikanaji wa viongozi katika ngazi ya Vitongoji, Vijiji na Mitaa.

Tatu, tunaendelea kufuatilia fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na Serikali ili ziweze kutumika kutokana na malengo yaliyokusudiwa pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa wanaofuja na kufanya ubadhirifu wa mali za umma.

Nne, tunaendelea na utekelezaji wa programu ya **TAKUKURU RAFIKI** kwa kufikia kata ambazo bado hazijafikiwa kwa ajili ya kubainisha kero mbalimbali zinazowakabili wananchi na kuzitafutia ufumbuzi kwa kuwekeana mikakati na wahusika.

MWISHO,

Ninawakumbusha pia kwamba, mwananchi yoyote anapohitaji huduma katika ofisi za Umma asikubali kutoa rushwa kama kishawishi cha kupatiwa huduma hiyo kwani huduma katika Ofisi za Umma hutolewa bure na pale ambapo huduma hiyo inatakiwa kulipiwa, utaratibu ufuatwe ikiwa ni pamoja na kupatiwa stakabadhi kuhusiana na malipo yaliyofanyika.

Ninatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kufika katika ofisi zetu ambazo ziko kila wilaya.

Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu; Tutimize Wajibu Wetu

....Ninawashukuru sana kwa kunisikiliza...

Imetolewa na:

Manyama Tungaraza,
Mkuu wa TAKUKURU (M)
MOROGORO.
0738150143

KIAMBATANISHO 1. UFURATILIAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

Na	JINA LA MRADI	KILICHOBAINIKA	HATUA ILIYOCHUKULIWA
1.	Umaliziaji wa Bweni la wavulana Shule ya Sekondari Lupiro, Halmashauri ya Wilaya Ulanga wenye thamani ya Shilingi **20,000,000.00**	Ucheleweshaji wa ukamilishaji wa mradi.	Elimu na ushauri juu ya usimamizi wa mradi ilitolewa kwa wajumbe wa Kamati ya Ujenzi.
2.	Uimarishaji wa huduma za rufaa na ubora wa huduma za afya msingi, Halmashauri ya Wilaya Kilosa wenye thamani ya Shilingi **21,085,821.46**	Matumizi ya fedha pasipo uzingativu wa taratibu	Elimu ya uzingatiaji wa matumizi ya fedha umetolewa kwa wasimamizi wa mradi.
3.	Ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya halmashauri ya Mji Ifakara wenye thamani ya Shilingi **500,000,000.00**	Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi.	Uchunguzi umeanzishwa
4.	Ujenzi wa shule mpya ya sekondari Lipangalala, Wilaya Kilombero wenye thamani ya Shilingi **528,000,000.00**	Taratibu za zabuni hazikuzingatiwa	Uchunguzi unaendelea
5.	Ujenzi wa mabweni na madarasa shule ya sekondari Ifakara, Wilaya Kilombero wenye thamani ya Shilingi **470,000,000.00**	Uchelewaji wa ulipaji wa fedha toka kwa mfadhili BARICK GOLD MINING.	Ufuatiliaji unaendelea kufanyika.
6.	Ujenzi wa madarasa 7 ya msingi, madarasa 2 ya awali, jengo la utawala, vyumba vya utawala, matundu 8 ya vyoo, vya shule ya msingi na matundu 6 ya awali Pamoja na kichomea taka- shule ya msingi Njiwa, Wilaya ya Malinyi wenye thamani ya Shilingi **306,900,000.00**	kutokumalimika kwa baadhi ya kazi husuani za uwekaji wa tiles	Ushauri yametolewa kwa mkuu wa shule kusimamia marekebisho ya kazi zilizobaki
7.	Ujenzi wa madarasa 2 na matundu ya vyoo 4 katika shule ya msingi Kiswago, Wilaya ya Malinyi wenye thamani ya Shilingi **51,200,000.00**	Baadhi ya kazi kutokukamilika hususani upakaji rangi kwenye mbao.	Mkuu wa shule ameshauriwa kuhakikisha mradi unakamilika
8.	Ufuatiliaji wa Mradi wa maji Turiani, Halmashauri ya Wilaya Mvomero wenye thamani ya Tsh **3,905,699,196.00**	➢ Kasi ndogo ya mkandarasi katika utekelezaji wa mradi ➢ Uwezo mdogo wa kifedha wa mkandarasi ➢ kazi kuchelewa	Mkandarasi kupewa semina ya usimamizi bora wa mradi huo na pia kutakiwa kurekebisha mapungufu yote yaliyobainika

		kukamilika ndani ya muda uliopangwa kutokana na uzembe wa mkandarasi	
9.	Ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa madarasa nane (8) ofisi mbili (2) maabara mbili (2) maktaba mmoja (1) na jengo la utawala Shule ya Sekondari Kweuma wenye thamani ya Tsh **528,425,000.00**	➢ kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi ➢ Usimamizi hafifu wa watendaji	Mwalimu mkuu kupewa semina ya usimamizi bora wa miradi na kushauriwa kurekebisha mapungufu yote yaliyobainika
10	ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu (**Two in one**) shule ya msingi Kaole wenye thamani ya Tsh **50,000,000.00**	➢ Ujenzi kutokamilika kwa muda uliopangwa ➢ Fedha imeisha kabla ya ukamilishaji wa mradi	Mwalimu mkuu wa shule ya Msingi Kaole kupewa semina ya usimamizi bora wa miradi na pia kushauriwa kurekebisha mapungufu yote yaliyobainika.
11	Ujenzi wa Majosho vijiji vya kibedya, Chakwale, Ngayaki, Kilama na Chogoali, Halmashauri ya Wilaya Gairo wenye thamani ya Tsh **114,500,000.00**	➢ Mkandarasi kulipwa kabla hajasupply vifaa ➢ Mkandarasi kuleta robo ya vifaa alivyoelekezwa ➢ Maafisa ugani kuchagua mzabuni kutoka Dar es Salaam bila kufanya ushindanishi wa wazabuni ➢ Majosho matatu kati ya matano ndio yamejengwa na bado hawajamalizia. Mzabuni hajaleta vifaa vilivyobaki	Mzabuni ameshauriwa kusimamia majosho yote yaishe ikiwa ni pamoja na kumlipa fundi na kuleta vifaa vyote site Uchunguzi umeanzishwa juu ya matumizi mabaya ya nyaraka kumdanganya mwajiri. Mashaihidi wote wamehojiwa, nyaraka zimepatikana kutoka Wizara ya Uvuvi na Mifugo na wahusika wamechukuliwa sampuli na zipo Makao Makuu.
13.	Ujenzi wa Shule ya Sekondari Lukande, Halmashauri ya Wilaya Ulanga wenye thamani ya Tsh **52,899,424**	Uchelewezaji wa ukamilishaji wa ujenzi	Kutoa ellimu wa wasimamizi pamoja na ushauri yametolewa kwa fundi ujenzi ili waweze kukamilisha ujenzi kwa wakati
14.	Ujenzi wa shule ya sekondari Madoto wilayani KILOSA shilingi 55,336,000.00	Mabati kutokuwa na ubora unaotakiwa kwa mujibu wa TBS	Mzabuni alishauriwa kurejesha gharama zote kuhusiana na ununuzi wa mabati, kofia na misumari na pia kurejesha vifaa vyake

			vya ujenzi ambavyo havikuwa na ubora
15.	Ujenzi wa shule ya sekondari Ruhembe Wilayani Kilosa Shilingi 69,214,500.00	Mabati kutokuw na ubora unaotakiwa kwa mujibu wa TBS	Mzabuni alishauriwa kurejesha gharama zote kuhusiana na ununuzi wa mabati, kofia na misumari na pia aliagizwa kuchukua vifaa vyote ambavyo havikuwa na ubora unaotakiwa.

KIAMBATANISHO 2. UCHAMBUZI WA MIFUMO

Na.	Uchambuzi wa mfumo	Kilichobainika	Hatua iliyochukuiwa
1.	Uchambuzi wa mianya ya rushwa katika mfumo wa huduma za sekta ya ardhi, Halmashauri ya Mji ifakara.	Kutokuzingatiwa kwa Sheria, taratibu na miongozo katika utoaji wa huduma Sekta ya Ardhi	TAKUKURU inatarajia kuandaa kikao/ warsha kwa ajili ya kuweka maazimio ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika.
2.	Udhibiti wa mianya ya rushwa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi katika mabaraza ya kata wilaya ya Ulanga.	Kutozingatiwa kwa taratibu za fedha katika shughuli za mabaraza.	Kuwasilisha mapendekezo katika warsha na wadau ili kujadili na kuwekeana maazimio kwa ajili ya kupata mwongozo wa kuendesha Mabaraza ya Kata.
		Kuwepo kwa tofauti kubwa ya gharama za kufungua kesi kati ya baraza na baraza.	
3.	Uchambuzi wa mfumo wa huduma za ardhi katika Halmashauri ya wilaya ya Ulanga.	Kutozingatiwa kwa mkataba wa huduma kwa wateja wa wizara ya ardhi na maendeleo ya makazi	Kuwasilisha mapendekezo katika warsha na wadau ili kuwekeana maazimio kuhusiana na changamoto zilizopo ya namna ya kuzitatua
4.	Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa minada ya mifugo katika Halmashauri ya wilaya ya Ulanga	Halmashauri ya Wilaya kutowekeza katika minada kwa kutengeneza miundombinu ya kuongeza ufanisi wa minada.	Kuwasilisha mapendekezo katika warsha na wadau wadau ili kujadili changamoto zilizobainika na kuwekeana maazimio ya namna ya kuzitatua.
		Vijiji vyenye minada kutonufaika na mapato ya minada hiyo.	
		Kutokuwepo kwa mikataba ya kisheria juu ya ardhi ya vijiji ambayo hutumiwa na Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya minada.	

KIAMBATANISHO 3. MREJESHO WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

Na	Sekta	Kero	Jawabu la kero
1.	**Elimu**	Walimu wanaoripoti katika Shule za Msingi za Kata ya Nyandira – Wilayani Mvomero, mara nyingi hawarudi katika Shule hizo na badala yake huonekana kupangiwa Shule tofauti na ile ya mwanzo.	Idara ya elimu ya awali na Msingi inafuatilia kujua walimu waliopangwa kata ya Nyandira na baadaye kuhamishwa.
2.	**Barabara**	Wakandarasi hawatoi taarifa kwa viongozi wa Kata na Vijiji wanapotekeleza ujenzi wa Barabara- Wilaya ya Mvomero	Katika miradi ya TARURA ushirikishwaji hufanyika katika eneo husika mfano barabara ya N**yandira - Tchenzema** iliyotekelezwa na Mkandarasi M/S **GWEMA GENERAL ENTERPRISES COMPANY LTD** Wananchi wameshirikishwa.

KIAMBATISHO 4. TAKUKURU RAFIKI

Mifano ya Kero Kisekta na Namna Zilivyotatuliwa	Utatuzi wa kero
1. MALIASILI- Kuwepo kwa Wanyama aina ya tembo maeneo ya Ngerengere na kusababisha athari kwa wananchi waishio maeneo hayo.	**TAWA** wanatakiwa kufika katika maeneo hayo na kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kutatua tatizo hilo la wanyama kuvamia makazi ya watu na kuharibu mazao yao.
2. LATRA- Hakuna huduma ya usafiri kutoka Ubena hadi Ngerengere; Kutokuwepo kwa bei elekezi kwa nauli za magari kwenye kata ya Tununguo ambapo ilipelekea nauli kufikia Sh. Elfu kumi na nne (14,000/=) kutoka Tununguo hadi Ubena.	LATRA Morogoro wameeleza kwamba nauli kati ya Tununguo hadi Ubena itapangwa baada ya kupata umbali wa Kilometa katika eneo hilo. Aidha huduma ya usafiri kati ya Ubena na Ngerengere upo kuna Hiace 3 na pia kuna Noah ambazo zinatoka Chalinze Kwenda Ngerengere.
3. ARDHI- Taasisi za Serikali zinazotoa huduma za kijamii kama vile shule na kituo cha afya zilizopo maeneo ya Tununguo hazijarasimishwa na kupimwa.	Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri imeelekezwa na itapima maeneo hayo na kutengeneza Hati.
4. ELIMU – Kutokukukamilika kwa vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi Sinyaulime, Zumbu, Kiwege na Njianne	Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri imeeleza kwamba Kuna idadi kubwa ya majengo ya shule ambayo yapo katika hatua ya boma ikilinganishwa na bajeti iliyopo kwa ajili ya umaliziaji wa majengo hayo. Ukamilishaji wa maboma hayo utafanyika hatua kwa hatua kwa kuzingatia upatikaji wa fedha.
5. AFYA- Wajawazito kutokupata stakabadhi za malipo ya faini wanazotozwa katika zahanati ya Italagwe kutokana na kujifungulia nyumbani.	Mganga mfawidhi wa zahanati ya Italagwe aliagizwa na TAKUKURU kuhakikisha wanatoa stakabadhi kwa akinamama kwa ajili ya malipo ya faini na kutoa taarifa kila mwezi TAKUKURU.
6. MIFUGO- Vijiji kutokuwa na mapito ya mifugo kwa ajili ya kwenda malishoni.	Wenyeviti wa vijiji na vitongoji waliagizwa na TAKUKURU kuitisha mikutano ya wananchi na kukubaliana kutenga njia za mifugo kupita wakati wa kwenda malishoni.
7. Elimu: Walimu wakuu kuchukua Vyakula vya wanafunzi mashuleni kwa matumizi yao binafsi.	TAKUKURU iliwaagiza walimu wakuu wote wa shule za msingi na sekondari kutojihusisha na ukusanyaji wa chakula kutoka kwa wazazi kwa ajili ya wanafunzi badala yake wazazi wenyewe waunde kamati ya kusimamia masuala ya chakula katika shule zao.
8. LISHE - Kukosekana mpango wa lishe shule za kata ya Lupiro	Afisa Mtendaji Kata ya Lupiro amelekezwa kuweka na kusimamia mpango wa lishe shule zote za kata ya Lupiro.